JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

PARLIAMENT
OF KENYA
LIBRARY

KAMATI YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA BIASHARA

---

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA BIASHARA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI NA MADININ KWA MWAKA WA FEDHA 2006/2007

---

OFISI YA BUNGE
S.L.P. 941
DODOMA

17 JULAI 2006

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA BIASHARA

---

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA BIASHARA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI NA MADININ KWA MWAKA WA FEDHA 2006/2007

---

KENYA NATIONAL ASSEMBLY
Accession: 10014133
Call No: 352.4 | BLT

OFISI YA BUNGE
S.L.P. 941
DODOMA

17 JULAI 2006

# TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA BIASHARA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2006/07

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani zangu kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa Taarifa, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2006/07 kwa mujibu wa Kanuni Na.81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2004.

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kusema kwamba naiunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara (INTRA) ambao ndio waliochambua Bajeti ya Wizara hii kwa umakini na ufanisi mkubwa , nao ni:-

| | | |
|---|---|---|
| 1.1 | Mhe. William H. Shellukindo, Mb. | Mwenyekiti |
| 1.2 | Mhe. Dk.Harrison G.Mwakyembe,Mb | M/Mwenyekiti |
| 1.3 | Mhe. Mohammed A. Chomboh, Mb. | Mjumbe |
| 1.4 | Mhe. Yahya K. Issa, Mb. | " |
| 1.5 | Mhe. Asha M. Jecha, Mb . | " |
| 1.6 | Mhe. Siraju J. Kaboyonga, Mb. | " |
| 1.7 | Mhe. Mwajuma H. Khamis, Mb | " |

| | | |
|---|---|---|
| 1.8 | Mhe. Vuai A Khamis, Mb. | « |
| 1.9 | Mhe. Mhe. Fuya G. Kimbita, Mb. | " |
| 1.10 | Mhe.Eng. Stella M. Manyanya, Mb. | " |
| 1.11 | Mhe. Fatma A. Mikidadi, Mb. | " |
| 1.12 | Mhe. Herbert J. Mntangi, Mb. | " |
| 1.13 | Mhe. Mohammed H. Mnyaa, Mb. | " |
| 1.14 | Mhe. Luhanga Joelson Mpina, Mb. | " |
| 1.15 | Mhe. Mbaruk K. Mwandoro, Mb. | " |
| 1.16 | Mhe. Saverina Silvanus Mwijage, Mb | " |
| 1.17 | Mhe. Dk. Lucy S. Nkya, Mb. | " |
| 1.18 | Mhe.Christopher O. Ole-Sendeka, Mb | " |
| 1.19 | Mhe. Lucy F. Owenya, Mb. | " |
| 1.20 | Mhe. Ahmed Ally Salum , Mb | " |
| 1.21 | Mhe. Haji J. Sereweji, Mb | " |
| 1.22 | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb | " |
| 1.23 | Mhe. Mohammed S. Sinani, Mb | " |
| 1.24 | Mhe. Abdallah Salum Sumry, Mb. | Mjumbe. |

2.0 **Mheshimiwa Spika,** kama ilivyo kawaida wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara, Kamati ilizingatia vipengele vifuatavyo kuhusu Fungu 58: Wizara ya Nishati na Madini.

2.1 Dira/Mwelekeo wa Wizara kuhusu kushughulikia masuala ya nishati na madini nchini.

2.2 Majukumu ya Wizara.

2.3 Taarifa kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara katika Mwaka 2005/06.

2.4 Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Mwaka 2005/06.

2.5 Maelezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2005/06.

2.6 Maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2006/07.

## 3.0 KUPITIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA NA USHAURI ULIOTOLEWA WAKATI WA MCHAKATO WA BAJETI YA 2005/06

**Mheshimiwa Spika,** tunapenda kuipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali ilizozifikia katika kutekeleza ushauri wa Kamati. Pia Wizara imejitahidi kwa kiasi kikubwa kutekeleza malengo ya shughuli ilizojipangia katika hali ya ufinyu wa Bajeti na hasa kutokana na kupunguzwa kwa fedha zilizotengwa ili kukabili janga la njaa na ukame uliosababisha kupungua kwa maji kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme.

**Mheshimiwa Spika** hapa napenda niipongeze Serikali kuhusu yafuatayo:-

### 3.1 Shirika la Taifa la Mafuta ya Petroli (TPDC):

Kamati imefurahishwa na juhudi zinazofanywa na Serikali kwa kutambua upeo na uwezo wa TPDC na kuutumia kama ilivyoonekana katika bajeti ya mwaka huu 2006/2007 ambapo Wizara imetengewa Sh.6.2

bilioni chini ya Bajeti ya Maendeleo Fungu 58, Kifungu 3001-3115,(Petroleum Sub sector Development). Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizo kadri zinavyohitajika; kwa sababu miaka iliyopita fedha zilitengwa lakini hazikutolewa.

- **Mheshimiwa Spika**,Kutokana na kupanda kwa bei za nishati ya mafuta katika soko la dunia na mahitaji ya nishati mbadala nchini, Shirika litatakiwa kufanya shughuli nyingi na kwa uharaka. Shughuli za Utafiti ni muhimu sana kwa vile kuna kila dalili za kuwepo Mafuta na Gesi Asilia kwa wingi nchini, hivyo ni vizuri kuongeza kasi ya utafiti na kuipatia TPDC uwezo wa kushirikiana na wawekezaji katika sekta hii.

- **Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa Serikali wa kuipatia TPDC nafasi ya ghorofa saba katika sehemu mojawapo ya Jengo la Mafuta (Mafuta House), pamoja na sehemu ya chini kwa ajili ya kuhifadhia sampuli za miamba na takwimu za utafiti wa mafuta, ni hatua nzuri ya kuthamini shughuli za Shirika hilo. Ni matumaini ya Kamati kwamba TPDC katika jengo husika haitaonekana kuwa ni mpangaji bali mmiliki mwenza wa jengo hilo na hivyo halitatozwa kodi ya pango la sehemu hiyo.

- **Mheshimiwa Spika**, Ili TPDC isionekane kama inafadhiliwa na pia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), wapewe hisa zinazolingana na thamani ya gharama walizotumia katika ujenzi wa Jengo hilo (Mafuta House). Vilevil, ili kujua gharama halisi za Shirika la Hifadhi ya Taifa (NSSF) katika kukamilisha jengo hilo,ifanyike tathmini na mtaalam wa majengo ili kuondoa viwingu vya mashaka.

- **Mheshimiwa Spika,** pia Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali wa kulipa Shirika la Mafuta uwezo ili kuongeza idadi ya hisa zake kwa niaba ya Serikali katika Kampuni ya "*Pan-African Energy*". Uamuzi huo utaiwezesha Serikali kupata gawio kubwa kutokana na faida inayopatikana kutokana na mauzo ya Gesi Asilia kuliko ilivyo sasa. Vilevile Kamati inashauri kwamba, uamuzi huo utekelezwe mapema kwa kuipatia TPDC kiasi cha fedha zitokanazo na mauzo ya Gesi Asilia ya Songo Songo kwa ajili ya ushiriki wake katika utafiti na kuendeleza mradi wa Gesi.

## 3.2 Mitambo ya Independent Power Tanzania Ltd ( IPTL)

- **Mheshimiwa Spika,** wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2005/06, Kamati iliishauri Serikali iharakishe mazungumzo yatakayowezesha

Serikali kununua mitambo ya kuzalisha umeme ya IPTL Tegeta ili Taifa liweze kuepukana na gharama za malipo ya uwezo wa kuzalisha umeme ( *capacity charges)*.Kamati inaendelea kushauri kwamba Serikali inunue mitambo hiyo.

- Aidha,kuhusu uamuzi wa Serikali kuibadili mitambo hiyo ili iweze kutumia Gesi Asilia badala ya Mafuta Mazito, Kamati inaupongeza uamuzi huo kwa vile utapunguza gharama za uzalishaji. Na ni matumaini ya Kamati kwamba baada ya kubadilisha mfumo huo wa mafuta mazito na kutumia Gesi,gharama za umeme nazo zitapungua maana gesi ina gharama ndogo.

### 3.3 SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA ( STAMICO):

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifurahishwa na azma ya Wizara kuliendeleza na kulipa uwezo zaidi Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kumudu majukumu yake kwa ufanisi zaidi na hasa jukumu la kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini. Kamati inashauri kwamba suala la kuwaendeleza na kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini lipewe kipaumbele maalumu katika mwaka wa fedha 2006/07 ili kuwapunguzia adha wahangaikaji hao.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2006/2007 Wizara ya Nishati na Madini inaomba fedha chini ya Fungu 58 kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4.1 | Fedha za Matumizi ya Kawaida | - | Tsh. 32,657,178,000/= |
| 4.2 | Fedha za Matumizi ya Maendeleo | - | Tsh.432,544,995,000/= |
| | **Jumla** | - | **Tsh.465,202,173,000/=** |

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia na kuchambua kwa makini Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini na kuridhika na kazi zitakazotekelezwa katika kipindi kijacho, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

5.1 Kupatikana kwa Gesi Asilia Tanzania ni ukombozi mwingine ambao Mwenyezi Mungu ametujalia. Kamati inapenda kulipongeza Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) ambalo lilikamilisha utafiti na kugundua kuwa nchini ipo Gesi Asilia na ambayo inaweza kuvunwa kibiashara.

Kinachotakiwa sasa ni kuhakikisha kwamba utafiti unaongezewa nguvu kwa lengo la kugundua Gesi Asilia nyingine zaidi.

Kazi hii iende sambamba na kuifikisha gesi hiyo mapema kule inakohitajika. Kwa sasa wenye viwanda wengi hapa nchini, Jijini Dar-es-Salaam na nje ya Dar-es-Salaam na hata nje ya nchi wangependa kutumia nishati ya gesi katika michakato yao ya uzalishaji.

- **Mheshimiwa Spika**,kwa upande mwingine, Serikali ifanye maamuzi ya haraka kuhusu matumizi zaidi ya rasilimali hiyo kama vile matumizi ya kupikia majumbani na kuendeshea magari. Aidha, matumizi hayo ya gesi asilia yaende sambamba na kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waweze kukubali kutumia gesi badala ya mkaa. Pia, Serikali iweke vivutio maalum kwa wawekezaji katika shughuli za gesi na vifaa vinavyotumia gesi.

- **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Gesi ya Mnazi Bay kufanyike utafiti wa uwezekano wa gesi hiyo kutumika pia katika uzalishaji wa mbolea za chumvichumvi na bidhaa za nyingine.

- **Mheshimiwa Spika**,yapo malalamiko toka kwa baadhi ya Wateja kuwa bei ya gesi hiyo iko juu kwa vile upangaji bei zake umeegemea kwenye bei za mafuta katika soko la dunia. Ni vema bei hizo zikaangaliwa ili ziwe kivutio kwa watumiaji bila kuwepo hasara kwa wawekezaji husika.

## 5.2 Utafutaji wa Mafuta Nchini:

- **Mheshimiwa Spika,** Tafiti za mafuta hapa nchini zina historia ya miaka mingi na hatua kadhaa za mafaniko zimefikiwa. Kutokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, nchi nyingi sasa zinafanya tafiti nyingi za Nishati hiyo. Hapa nchini, maeneo kadhaa yametengwa kwa ajili ya tafiti hizo.

- Hata hivyo, kumekuwa na tatizo la kufanya tafiti katika eneo liitwalo "Block 12"; eneo hilo linaanzia kusini na linaendelea hadi sehemu ya Pwani ya Kisiwa cha Pemba. Kampuni iliyokodishiwa eneo hilo tangu mwaka 1998 hadi sasa haijaruhusiwa kuendelea na utafiti kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijaidhinisha zoezi hilo liendelee kutokana na rai ya kutaka kuangalia upya makubaliano ya ushirikiano kati yake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa masuala ya mafuta.

- **Mheshimiwa Spika**, linalojitokeza sasa ni kana kwamba Serikali inataka kuvunja mkataba na Kampuni iliyopata kibali cha kufanya utafiti na hivyo kuna uwezekano wa Kampuni hiyo kuishitaki Serikali kwa kuvunja mkataba huo. Kwa hiyo,

Kamati inaendelea kutoa rai kwamba rasilimali ya Mafuta ni mali ya Watanzania wote, hivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikae pamoja ili kupata muafaka kuhusu suala hilo na kuwezesha utafiti kuanza bila kuchelewa zaidi.

- **Mheshimiwa Spika**, Kamati inazipongeza Serikali zote mbili kwa hatua za mwanzo zinazochukuliwa zenye lengo la kuondoa utata uliopo.

### 5.3 Upungufu wa maji katika Mitambo ya Umeme inayoendeshwa na Maji:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika ziara zake ilifahamishwa baadhi ya sababu zinazosababisha tatizo kubwa katika mitambo ya umeme wa maji. Sababu hizo ni pamoja na ukame, wananchi kutumia maji kwa ajili ya kumwagilia mashamba yao pamoja na kulichunga mifugo kwenye vyanzo vya maji.

Kamati inashauri kwamba hatua madhubuti zichukuliwe ili mtiririko wa maji kuelekea kwenye mitambo ya umeme usiingiliwe pamoja na kuchukua hatua kali kwa wale wote watakaokiuka maagizo ya Serikali ya kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji.

5.4 **Usambazaji wa Umeme:**

- **Mheshimiwa Spika,** Wizara hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba watumiaji wa umeme wanaupata ipasavyo na kwa gharama nafuu. Tunaipongeza Serikali kwa mpango wake wenye malengo kwamba ifikapo mwaka 2025 Makao Makuu yote ya Wilaya yatakuwa yamefikishiwa umeme na hatimaye Makao Makuu yote ya majimbo ya Uchaguzi.

- **Mheshimiwa Spika**, Waziri wa Nishati na Madini katika mpango wa maendeleo, ameorodhesha Miji kadhaa ambayo itapatiwa umeme mwaka huu. Vile vile ameonyesha matumaini kwamba Miji mingine 18 itaombewa fedha kupitia mpango wa "Millenium Challenge Account" unaofadhiliwa na Marekani. Kamati inapongeza juhudi hizo maana kuna matumaini kwamba mpango huo utasaidia kupunguza muda wa kufikiwa kwa lengo lililowekwa.

5.5 **Miradi ya Chuma Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma:**

- **Mheshimiwa Spika,** ahadi ya Waziri ya kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya haitafanikiwa kama hakutakuwa na ongezeko la

uzalishaji wa umeme. Kamati inasikitika kwamba Uwekezaji katika miradi ya Chuma Liganga na Mkaa wa Mawe Mchuchuma umekuwa kitendawili. Kwa bahati nzuri, Kamati hii ilipata fursa ya kutembelea maeneo hayo mwezi Aprili 2006.

- **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kuamini kwamba miradi hii miwili haiwezi kuanza kwa pamoja kwani Mradi wa Chuma Liganga unategemea kwanza kuwepo kwa umeme wa kutosha kiasi cha megawati (megawatts) 200. Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba mradi wa Mchuchuma uanze kwanza ili uweze kuzalisha umeme. Inasemakana kuwa mradi huo una uwezo wa kuzalisha hadi megawati (Megawatts) 1,600 za umeme, lakini utaanza kwa kuzalisha megawati (Megawatts) 200 na kuendelea kwa awamu.

- **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imeelezwa kuwa Makampuni kadhaa ya ndani na nje ya nchi yameomba kuwekeza katika mradi huo. Kamati inapenda kusisitiza kwamba mchakato wa kuipata Kampuni mahiri kwa ajili hiyo uanze mara moja na kwamba mwekezaji huyo apatikane kwa kuzingatia yafuatayo:-

    (a) Uwazi katika kuitisha na kuteua mwekezaji/wawekezaji .

(b) Uwezo wa kitaalam wa kuweza kuchimba na kuchenjua madini aina mbalimbali yatakayochimbwa.

(c) Uwezo kifedha, na

(d) Uzoefu katika kufanya shughuli hizo.

- **Mheshimiwa Spika,** Kamati ingependa ieleweke kwamba madini yaliyoko Liganga si chuma pekee bali pia yapo madini mengine kama *Venadium* na *Titenium* ambayo thamani yake ni kubwa duniani kuliko hata hicho chuma.

- **Mheshimiwa Spika**, kutozingatia vigezo hivyo na kukubali mashinikizo mbalimbali Taifa linaweza kupata hasara kubwa. Ni vizuri ikaeleweka kwamba rasilimali hizo si za wananchi wa Ludewa peke yao, bali ni rasilimali ya Watanzania wote. Kuna miradi mikubwa ya uchimbaji madini Wilaya za Kahama, Geita, Shinyanga, Simanjiro, Tarime n.k. Wananchi wa Wilaya hizi wamekubali ukweli huu, kwa nini wengine wafanye tofauti. Hata hivyo Kamati, kama ilivyo kwa wananchi wa Ludewa, inapenda uwekezaji katika mradi huo uanze haraka iwezekanavyo, ili Taifa kwa jumla linufaike wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Ludewa.

## 5.6 Kutumia Malighafi Mbalimbali Katika Kuzalisha Umeme:

- **Mheshimiwa Spika,** Kwa miaka mingi iliyopita kulikuwa na umeme uliozalishwa kwa mafuta na baadaye ukapatikana umeme unaozalishwa kwa maji, hali iliyowezesha kuuweka umeme huo kwenye Mtandao wa Kitaifa (National Grid).

- **Mheshimiwa Spika**, umeme sasa unazalishwa kwa kutumia Gesi Asilia pamoja na Makaa ya Mawe. Pia kuna vyanzo vingine kama vile magome ya miwati Wilayani Njombe n.k. Kila kimoja cha vyanzo hivi kikitumiwa pekee hakitatosheleza mahitaji ya Umeme nchini. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali iangalie utaratibu wa kutumia vyanzo vyote kwa pamoja ili kukidhi mahitaji.

- **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Kampuni ya Mkaa wa Mawe ya Kiwira (Kiwira Coal Mines Ltd.) kwa kuwa tayari imeanza kuzalisha umeme wa wa ziada na kuliuzia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Kampuni hiyo imepanga kuendelea kuzalisha megawati (Megawatts) 200 za Umeme katika awamu ya kwanza na baadaye kufikia megawati ( Megawatts) 400.

## 5.7 Machimbo ya TANZANITE Mererani:

- **Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ilipata fursa ya kutembelea Machimbo ya Vito vya TANZANITE huko Mererani Wilayani Simanjiro. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea Wachimbaji wadogo pamoja na wachimbaji wakubwa wa Kampuni ya TANZANITE ONE. Katika mikutano tuliyofanya na wachimbaji hao kila upande kati ya pande hizi mbili ulikuwa unalaumu upande mwingine. Pia kulikuwa na malalamiko ya wachimbaji kukutana kati ya vitalu na vitalu (blocks) huko ardhini. Wachimbaji wenyewe wanaita kutobozana.

Ili kumaliza matatizo hayo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

5.7.1 Kwa ujumla, maeneo wanayogawiwa wachimbaji wadogo ni madogo mno na ndio sababu ya kukutana huko ardhini. Maeneo hayo yana ukubwa wa mita 50 x 50. Hivyo, Kamati inashauri kwamba wachimbaji hao washawishiwe kujiunga katika makundi ili kwa pamoja waweze kugawiwa maeneo ya kutosha na kuondoa tatizo la kutobozana.

5.7.2 Kwa kutambua kuwa nchi nyingi duniani hazitoi Leseni za kuchimba vito kwa wageni , kwa mfano nchi za India,Malawi n.k Kamati inashauri kwamba Serikali isitoe leseni nyingine mpya wala kuongezewa maeneo kwa Kampuni za kigeni na pia kwa kampuni za Kitnzania zilizopo, pindi leseni hizo zikiisha muda wake.

5.7.3 Sheria ya Uchimbaji Madini ya Mwaka 1998 inayomtaka Mchimbaji wa madini aende chini moja kwa moja *(vertically)* iangaliwe upya kwa vile mara nyingi madini ya TANZANITE yanafuata mkondo na hivyo huenda mshazari *(Horizontally)*. Pamoja na kuongezwa kwa ukubwa wa vitalu, madini ya TANZANITE yatengenezewe kanuni zake tofauti na madini mengine.

5.7.4 **Kuwepo na Nyenzo za Kisasa:**

Kwa kawaida wachimbaji wadogo wanakwenda chini ya ardhi hadi Mita 200 tu. Huo ndio uwezo wao kutokana na nyenzo duni walizonazo.

Kamati inapendekeza kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwawezesha Wachimbaji hao wapate vifaa vitakavyowawezesha wachimbe kwenda chini zaidi na hivyo kupunguza uwezekano wa kutobozana.

5.7.5 Kuwepo na Soko la vito karibu na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KIA)*:

**Mheshimiwa Spika,** kutokuwepo na soko la uhakika kwa vito vya TANZANITE kumeifanya nchi ipoteze fedha nyingi kutokana na wanunuzi kununua vito hivyo kwa njia za magendo. Aidha, Wauzaji na wanunuzi wanakumbana na matatizo mengi yakiwemo ya kudhulumiana.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza kuwepo Soko la Vito (vito vya aina zote) na **lijengwe karibu na Mererani** yanapopatikana madini ya Tanzanite ambapo wanunuzi na wauzaji watakutana. Eneo la Mererani liko karibu na Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro. Na kwa mnunuzi wa nje ataruka na ndege hadi KIA na kununua vito kwa karibu na kuingia kwenye ndege bila hofu ya kunyang'anywa fedha au vito. Pamoja na faida hiyo ya kuwa na soko la vito, hali hiyo pia

itahamasisha shughuli nyingine za uchumi zinazoendana na madini ya vito.

### 5.8 Matumizi ya Umeme bila kulipia:

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na malalamiko kwamba baadhi ya watumiaji umeme hawalipii matumizi yao ya umeme kwa vile hawajulikani na TANESCO. Kamati inashauri Serikali kuiagiza TANESCO ianze kufunga mita za Luku kwenye miradi mipya yote. Hali hii itaimarisha ukusanyaji mapato ya TANESCO na kupunguza hasara kwa Shirika na kuwezesha Serikali kupata gawio.

### 5.9 Mikataba Katika Sekta ya Nishati na Madini

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na utata na viwingu vya mashaka kuhusu mikataba mbalimbali iliyoingiwa kati ya Serikali na Wawekezaji katika sekta ya nishati na pia ya madini kwamba baadhi ya vipengele vya mikataba hiyo vinakataza mikataba hiyo baada ya kusainiwa isionwe na mtu mwingine yeyote zaidi ya wale waliyoisaini. Hali hii inaleta wasiwasi kuhusu namna mikataba hii ilivyoingiwa.Kamati yangu inatambua kuwa Wizara au Serikali imeunda Tume kufuatilia mikataba mbalimbali iliyosainiwa chini ya Wizara kama ule wa IPTL ambao umekuwa ni mzigo

mkubwa sana kwa Taifa. Tume hiyo ya Serikali ni ya kiutendaji wa Serikali na itakuwa na muono wa Kiserikali na hivyo waendelee na kazi zao.

**Pendekezo kwa Bunge:**

**Mheshimiwa Spika,**kwa vile mikataba hii inahusu Taasisi za umma, Kamati hii inapendekeza kuwa Bunge lako Tikufu,kwa mujibu wa Kanuni Na.104 ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004 liunde **KAMATI TEULE** ili iweze kupitia mikataba mbalimbali ya sekta ya Nishati na Madini yenye utata na kutoa Taarifa Bungeni.

5.10 **Kuwepo na Akiba ya kutosha ya Mafuta (Strategic Oil/ Fuel Reserves)**

**Mheshimiwa Spika,** Mafuta yanayotumiwa hapa Nchini yote yanaagizwa na Wafanyabiashara binafsi na hivyo hata Serikali haina takwimu sahihi za mahitaji ya mafuta na matumizi yake hapa Nchini. Kwa hali hii, kama jambo lolote linaweza kutokea kwa upande wa wauzaji (suppliers) wa nje ya Nchi au kwa wafanyabiashara/ waagizaji na kufanya shughuli zinazotumia mafuta kusimama kwa muda hadi utaratibu mwingine wa haraka utakapofanyika. Ili kuepuka hali kama hiyo na kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta wakati wote; Kamati inashauri kuwepo na **Hifadhi ya Taifa ya Mafuta** ambayo

yataweza kutumika kwa siku kadhaa kwa mfano siku 45. Utaratibu huu unatumika katika Nchi nyingi duniani hivyo Nchi yetu iuanzishe.

## 5.11 Upandaji wa Bei za Mafuta Katika Soko la Ndani:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa Serikali inafanya kila jitihada ili kuhakikisha kuwa bei za mafuta nchini zinapungua. Kwa mfano katika Bajeti ya mwaka huu 2006/07, Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) lakini maamuzi hayo hayajashusha bei hizo. Hali hii inatokana na waagizaji wakubwa wa mafuta kuungana katika kupanga bei. Inawezekanaje wakati mwingine bei za mafuta Dodoma zinakuwa za chini kuliko za Dar es Salaam?

- Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kutoa leseni kwa waagizaji wengi wa mafuta ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu waagizaji hao kutumia maghala ya kuhifadhia mafuta ya kukodi. Pia kwa vile tayari sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Nishati na Maji (EWURA) ipo, ni vema Mamlaka hiyo ianze kazi haraka ili usimamizi wa sheria na matumizi ya maji na mafuta ya petroli,dizeli na mafuta ya taa uweze kufanyika na kudhibiti ongezeko la bei za mafuta na nauli za vyombo vya usafiri.

5.12 **Kuwepo Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano wa Nishati**

**Mheshimiwa Spika,** Suala la upatikanaji wa nishati ya kuaminika Nchini halijawekewa mkakati maalum. Mipango tuliyonayo kuhusu nishati ni ya kawaida tu kama ilivyo mipango mingine ya ujenzi wa barabara,uchimbaji wa visima vya maji. Kwa mfano katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 nishati kutokana na mkaa wa mawe wa Mchuchuma imesisitizwa lakini katika mpango wa maendeleo wa umeme Kusini mwa Afrika (SADC Countries) mchango wa umeme kutokana na mkaa wa mawe haujaonyeshwa. Hali hii haionyeshi umuhimu wa aina hii ya nishati.

- **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali iandae **Mpango Maalum wa Maendeleo wa Nishati wa Miaka Mitano na kuuwasilisha Bungeni** ili uweze kutengewa bajeti itakayokidhi mahitaji ya nishati nchini katika mwaka wa fedha ufuatao (2007/08).

## 6.0 HITIMISHO

6.1 **Mheshimiwa Spika,** namalizia kwa kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa Taarifa ya Kamati yangu kuhusu Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2006/07.

6.2 **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mb. Waziri wa Nishati na Madini; Mheshimiwa Lawrence Masha, Mb. Naibu Waziri wa Nishati na Madini; Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo na Mashirika chini yake kwa maandalizi mazuri ya taarifa zilizohitajika katika zoezi hili la kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na kwa ushirikiano wao mzuri na Kamati hii kwa wakati wote.

6.3 **Mheshimiwa Spika,** pia natoa shukrani nyingi kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo yoyote.
Napenda vilevile kuwashukuru Ndugu Aggrey N. Nzowa na Ndugu Abdallah Hancha kwa huduma nzuri walizotoa kwa Kamati hii kwa bidii wakati wote hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa wakati uliotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na Naunga Mkono Hoja.

Mhe. William H. Shellukindo, Mb.
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA**

**17Julai 2006**